TAARIFA YA KAWAIDA NA. 8931

**SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**
**(SURA YA 413)**

**AMRI**

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 19)*

AMRI YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI YA NAULI KIKOMO ZA ABIRIA WA DARAJA LA KAWAIDA KWA TRENI YA RELI YA KISASA NA. 01 YA MWAKA 2024

| | |
|---|---|
| Jina na tarehe ya kuanza kutumika | 1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini ya Nauli za Abiria kwa Daraja la Kawaida kwa Treni ya Reli ya Kisasa Na. 01 ya Mwaka 2024 na itaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. |
| | |
| Tafsiri | 2. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo: |
| | *"Mamlaka"* maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, kwa kifupi LATRA, iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413. |
| | *"Mtoa Huduma"* maana yake ni Shirika la Reli Tanzania, kwa kifupi TRC, iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Reli, Sura ya 170. |
| | "*nauli*" maana yake ni tozo ya usafiri inayolipwa na abiria au mwakilishi wa abiria kwa fedha taslimu au kwa njia ya kielektroniki kwenda kwa mtoa huduma au mwakilishi wa mtoa huduma ya usafiri wa abiria kwa treni ya reli ya kisasa aliyelipa mwenyewe au ailiyolipwa na mwakilishi wake. |
| | "SGR" ni kifupisho cha maneno *Standard Gauge Railway (yaani, Reli ya Kisasa).* |
| | "*Treni ya SGR*" ni treni inayotoa huduma kwenye SGR inayoendeshwa kwa kutumia nishati ya umeme. |
| | |
| Viwango vya nauli - treni inayosimama kila kituo | 3. Viwango vya ukomo wa nauli kwa kilomita viliyoidhinishwa kwa treni inayosimama kila kituo, kwa watu wazima na watoto wenye umri wa miaka 4 hadi 12, zimeainishwa katika Jedwali la Kwanza la Amri hii. |
| | |
| Viwango vya nauli kwa treni ya haraka | 4. Viwango vya ukomo wa nauli kwa kilomita viliyoidhinishwa kwa treni ya haraka (express train), kwa watu wazima na watoto wenye umri wa miaka 4 hadi 12, zimeainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii. |
| | |

| | |
|---|---|
| Nauli ya treni ya SGR inayosimama kila kituo | 5. Nauli kikomo za treni ya SGR zilizoidhinishwa kwa treni inayosimama kila kituo kwa watu wazima na watoto wenye umri zaidi ya miaka 12 zimeainishwa katika Jedwali la Tatu la Amri hii. |
| | 6. Nauli kikomo za treni ya SGR zilizoidhinishwa kwa treni inayosimama kila kituo kwa watoto wenye umri wa miaka 4 hadi 12, zimeainishwa katika Jedwali la Nne la Amri hii. |
| | |
| Nauli za treni ya SGR kwa treni ya haraka | 7. Nauli kikomo za treni ya SGR zilizoidhinishwa kwa treni ya haraka (express train) kwa watu wazima na watoto wenye umri zaidi ya miaka 12 zimeainishwa katika Jedwali la Tano la Amri hii. |
| | 8. Nauli kikomo za treni ya SGR zilizoidhinishwa kwa treni ya haraka (express train) kwa watoto wenye umri wa miaka 4 hadi 12, zimeainishwa katika Jedwali la Sita la Amri hii. |
| | |
| Masharti ya kuzingatia | 9. Masharti ya kuzingatia na Mtoa Huduma kabla ya kuanza kutumika kwa Nauli hizi ni:- |
| | (i) kuwa na leseni ya usafirishaji; |
| | (ii) kuwa na ithibati ya usalama wa miundombinu ya reli na mabehewa; |
| | (iii) kutumia mfumo wa utoaji wa tiketi za kielekroniki; |
| | (iv) kuunganisha mfumo wa tiketi za kieletroniki na mifumo ya LATRA; |
| | (v) kukokotoa malipo na utunzaji taarifa za abiria, nauli iliyolipwa, tiketi za kielektroniki zilizotolewa, kodi za Serikali na tozo za kisheria; |
| | (vi) kuwa na watumishi wa kada muhimu kwa masuala ya ufundi na uendeshaji wa treni ya SGR ikiwa ni pamoja na madereva waliothibitishwa na wahudumu waliosajiliwa na LATRA. |
| | |
| Maeneo ya Msingi ya kuzingatia | 10. Maeneo ya msingi ya kuzingatiwa na Mtoa Huduma kwa ufuatiliaji wa LATRA katika kutekeleza Amri hii ni pamoja na haya yafuatayo:- |
| | (i) Uzingatiaji nauli kikomo zilizoidhinishwa na LATRA kwa wakati wote; |
| | (ii) Matumizi ya mfumo wa tiketi za kieletroniki na kuunganisha mfumo huo na mfumo wa Mamlaka wa ufuatiliaji; |
| | (iii) Ukokotoaji na utunzaji wa kumbukumbu za malipo ya kodi za Serikali na tozo za udhibiti kwa mujibu wa Sheria na Kanuni; |
| | (iv) Kuoanisha taarifa za mahesabu ya abiria waliosafiri na mapato yaliyokusanywa ili kudhibiti upotevu wa mapato; |
| | (v) Kuweka mfumo wa usimamizi wa utoaji taarifa kwa wasafiri (Passenger Management Information System) na mfumo wa ufuatiliaji wa mwenendo wa treni (Train Tracking System); |
| | (vi) Kubandika nauli za safari ya kituo kwa kituo katika maeneo yanayoonekana na abiria kiurahisi kwa wakati wote; |
| | (vii) Kuhakikisha uwepo wa huduma bora kwa wateja ikiwemo mazingira ya vituo, usafi wa mabehewa, chakula na vinywaji, maji safi na salama, |

| | | |
|---|---|---|
| | | mwangaza wa kutosha, na kuweka utaratibu wa fidia dhidi ya majanga na upotevu wa mizigo ya abiria; |
| | (viii) | Kuzingatia vigezo vya usalama wa mabehewa na miundombinu ya reli kwa mujibu wa Sheria, Kanuni za Taratibu zilizopo; na |
| | (ix) | Kwa treni ya haraka (express train), kutosimama kwenye vituo zaidi ya vile vilivyoaidhishwa kwenye Amri hii, isipokuwa kwa idhini ya LATRA. |

---

**JEDWALI LA KWANZA**

---

(*Limetengenezwa chini ya amri ya 3)*

VIWANGO VYA NAULI KIKOMO KWA TRENI INAYOSIMAMA KILA KITUO KWA KILOMITA KWA WATU WAZIMA NA WATOTO

| Aina ya Huduma | Viwango Vilivyoidhinishwa (Shilingi) | |
|---|---|---|
| | Nauli ya Watu Wazima na Watoto wa zaidi ya Miaka 12 | Nauli ya Watoto wa Miaka 4 hadi 12 |
| Nauli ghafi ya kwa kilomita | 69.16 | 34.58 |
| Tozo ya udhibiti kwa kilomita | 0.35 | 0.18 |
| **Nauli itakayolipwa kwa kilomita** | **69.51** | **34.76** |

---

**JEDWALI LA PILI**

---

(*Limetengenezwa chini ya amri ya 4)*

VIWANGO VYA NAULI KIKOMO KWA TRENI YA HARAKA (EXPRESS TRAIN) KWA KILOMITA KWA WATU WAZIMA NA WATOTO

| Aina ya Huduma | Viwango Vilivyoidhinishwa (Shilingi) | |
|---|---|---|
| | Nauli ya Watu Wazima na Watoto wa zaidi ya Miaka 12 | Nauli ya Watoto wa Miaka 4 hadi 12 |
| Nauli ghafi ya kwa kilomita | 112.04 | 56.02 |
| Tozo ya udhibiti kwa kilomita | 0.56 | 0.28 |
| **Nauli itakayolipwa kwa kilomita** | **112.60** | **56.30** |

## JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya amri ya 5)*

NAULI KIKOMO ZA TRENI YA SGR KWA TRENI INAYOSIMAMA KILA KITUO KWA WATU WAZIMA NA WATOTO WENYE UMRI ZAIDI YA MIAKA 12

| Safari | | Umbali (Km) | Nauli (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| Kutoka | Kwenda | | Daraja la Kawaida |
| Dar es Salaam | Pugu | 19.0 | 1,000 |
| Dar es Salaam | Soga | 51.0 | 4,000 |
| Dar es Salaam | Ruvu | 73.0 | 5,000 |
| Dar es Salaam | Ngerengere | 134.5 | 9,000 |
| Dar es Salaam | Morogoro | 192.0 | 13,000 |
| Dar es Salaam | Mkata | 229.0 | 16,000 |
| Dar es Salaam | Kilosa | 265.0 | 18,000 |
| Dar es Salaam | Kidete | 312.0 | 22,000 |
| Dar es Salaam | Gulwe | 354.7 | 25,000 |
| Dar es Salaam | Igandu | 387.5 | 27,000 |
| Dar es Salaam | Dodoma | 444.0 | 31,000 |
| Dar es Salaam | Bahi | 501.6 | 35,000 |
| Dar es Salaam | Makutupora | 531.0 | 37,000 |

## JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya amri ya 6)*

NAULI KIKOMO ZA TRENI YA SGR KWA TRENI INAYOSIMAMA KILA KITUO KWA WATOTO WENYE UMRI WA MIAKA 4 HADI MIAKA 12

| Safari | | Umbali (Km) | Nauli (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| Kutoka | Kwenda | | Daraja la Kawaida |
| Dar es Salaam | Pugu | 19.0 | 500 |
| Dar es Salaam | Soga | 51.0 | 2,000 |
| Dar es Salaam | Ruvu | 73.0 | 2,500 |
| Dar es Salaam | Ngerengere | 134.5 | 4,500 |
| Dar es Salaam | Morogoro | 192.0 | 6,500 |
| Dar es Salaam | Mkata | 229.0 | 8,000 |
| Dar es Salaam | Kilosa | 265.0 | 9,000 |
| Dar es Salaam | Kidete | 312.0 | 11,000 |
| Dar es Salaam | Gulwe | 354.7 | 12,500 |
| Dar es Salaam | Igandu | 387.5 | 13,500 |
| Dar es Salaam | Dodoma | 444.0 | 15,500 |
| Dar es Salaam | Bahi | 501.6 | 17,500 |
| Dar es Salaam | Makutupora | 531.0 | 18,500 |

## JEDWALI LA TANO

(*Limetengenezwa chini ya amri ya 7)*

NAULI KIKOMO ZA TRENI YA SGR KWA TRENI YA HARAKA (EXPRESS TRAIN) KWA WATU WAZIMA NA WATOTO WENYE UMRI ZAIDI YA MIAKA 12

| Safari | | Umbali (Km) | Nauli (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| Kutoka | Kwenda | | Daraja la Kawaida |
| Dar es Salaam | Morogoro | 192.0 | 22,000 |
| Dar es Salaam | Dodoma | 444.0 | 50,000 |

## JEDWALI LA SITA

(*Limetengenezwa chini ya amri ya 8)*

NAULI KIKOMO ZA TRENI YA SGR KWA TRENI YA HARAKA (EXPRESS TRAIN) KWA WATOTO WENYE UMRI WA MIAKA 4 HADI 12

| Safari | | Umbali (Km) | Nauli (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| Kutoka | Kwenda | | Daraja la Kawaida |
| Dar es Salaam | Morogoro | 192.0 | 11,000 |
| Dar es Salaam | Dodoma | 444.0 | 25,000 |

TANBIHI: Mtoto mwenye umri chini ya miaka 4 hatalipa nauli. Hata hivyo, taarifa zao na wasafiri wengine wote zitatunzwa katika mfumo wa taarifa za abiria wanaosafiri kila siku.

Ahmed Mohamed Ame
MWENYEKITI WA BODI

Dodoma
10 Juni, 2024